# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. GEORGE SIMBACHAWENE (MB), KWENYE UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA AICC – JIJINI ARUSHA, FEBRUARI 06, 2024

---

***Mhe. Dadi Horace Kolimba****; Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha,*

***Ndg. Juma Mkomi;*** *Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma,*

***Dkt. Jasmine Tiisekwa;*** *Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Mhandisi. Benedict Ndombja;*** *Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Bw. Yusuf Hamad Rashid;*** *Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ),*

***Wakurugenzi*** *wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,*

***Wakuu wa Idara*** *za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali*

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo,*** *na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;*

***Waandishi wa Habari,***

*Mabibi na Mabwana;*

***Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametupa baraka ya uhai, afya na kibali cha sisi kuweza kukutana hapa leo, katika tukio hili muhimu la Kikao Kazi cha Nne (4) cha Serikali Mtandao.

Kwa namna ya kipekee, niwashukuru viongozi wote mliopo hapa kutoka sekta za umma na binafsi, kwa kujumuika nasi katika kufanikisha tukio hili. Hii inadhihirisha ushirikiano tulionao baina yetu sisi Serikali na Sekta binafisi, katika kuleta maendeleo ya taifa letu hasa katika jitihada za kukuza Serikali Mtandao. Niwapongeze na kuwasihi kudumisha ushirikiano huu kwa mustakabali wa maendeleo endelevu ya taifa na vizazi vyetu.

Vilevile, niishukuru na kuipongeza Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa ushirikiano wao na kufanya kazi kwa pamoja ili kuimarisha jitihada za Serikali Mtandao. Ushirikiano huo ndio umesaidia Mamlaka kufikia malengo inayojiwekea kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Natambua kuwa, viongozi hawa hawawezi kufanikiwa pasipokuwa na wasaidizi mahiri kwa maana ya Watumishi, ambao nao nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru, kwani kujitoa kwao ndiko kumepelekea kukamilika kwa kazi mbalimbali za Mamlaka, ikiwemo kuandaa na kuendesha kikao kazi hiki cha nne cha Serikali Mtandao.

Mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, nawashukuru ndugu zangu wanahabari kwani mmekuwa mabalozi wazuri wa kuifikishia jamii ya Watanzania na mataifa mengine ulimwenguni, kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Amiri Jeshi wetu, ***Rais wa Jamhuri ya Muungazo wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,*** katika kuijenga Tanzania ya kidijitali. Ni imani yangu kuwa mtaendelea na jitihada

hizi za kuitangaza vyema nchi yetu, hususan malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita, ya kuwezesha matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi wa Taasisi za Umma na utoaji wa huduma kwa wananchi kidijitali.

**Ndugu washiriki,** Mamlaka ya Serikali Mtandao ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019. Taasisi hii imepewa dhamana ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma.

Kuimarika kwa Taasisi hii kunatokana na nia ya dhati ya **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** ya kukuza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi wa Serikali na utoaji wa huduma kwa umma, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuupopote walipo..

**Ndugu washiriki,** Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), kwa pamoja zinatambua nafasi ya TEHAMA katika kufikia malengo ya Taifa, na hivyo kusisitiza juu ya matumizi sahihi ya TEHAMA katika

utekelezaji wa shughuli za Serikali na utoaji wa huduma kwa umma. Pamoja na mambo mengine, Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016, inasisitiza juu ya Serikali kutumia fursa zitokanazo na TEHAMA pamoja na matumizi sahihi na yenye tija ya Mifumo ya TEHAMA, katika kuboresha utendaji kazi wa Taasisi, unaosaidia kutatua changamoto za kiutendaji, kudhibiti mapato ya Serikali, kujenga na kuboresha uwezo, pamoja na kuimarisha mawasiliano miongoni mwa wadau wa Serikali..

Kwa kuwa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imepewa jukumu la kuratibu na kusimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini, niwahakikishie kwamba, Wizara itaendelea kulisimamia kwa weledi jukumu hili, ili kuhakikisha tunajenga Serikali ya Kidijitali kwa kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Sera na Sheria ya Serikali Mtandao.

**Ndugu washiriki**, Mhe. Rais ameelekeza kuhakikisha Mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma inawasiliana na kubadilishana taarifa kidijitali, ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi serikalini pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kama isemavyo kauli mbiu ya kikao kazi hiki ***"Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa ubadilishanaji salama wa taarifa"***, ni muhimu kuwa na mifumo pamoja na miundombinu ya TEHAMA inayozingatia Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili tuweze kubadilishana taarifa kidijitali na kwa usalama.

Mifumo ya TEHAMA inayozingatia Sheria na Viwango vya Serikali Mtandao, husaidia kupunguza urudufu wa mifumo na kuokoa fedha za Serikali. Hivyo, ni muhimu taasisi zote za umma kuzingatia sheria hii ili kuhakikisha usalama wa taarifa za Serikali, pamoja na kupunguza upotevu wa fedha za umma.

Katika kuhakikisha taasisi za umma zinabadilishana taarifa kama alivyoelekeza **Mhe. Rais,** e-GA imefanikiwa kujenga Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji taarifa Serikalini ***"Government Enterprises Service Bus – GoVESB",*** ambao unawezesha mifumo ya TEHAMA serikalini kubadilishana taarifa. Hivyo basi, pamoja na mambo mengine mtakayojadiliana katika kikao kazi hiki, ni muhimu kuweka mikakati ya kuhakikisha mifumo yote mtakayoianzisha katika taasisi zenu inakidhi sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao, ili iweze kubadilishana taarifa.

Lakini pia, ni muhimu kwa kila taasisi kuhakikisha imejiunga na mfumo huu wa **GoVESB** ili kubadilishana taarifa na taasisi

nyingine, kama ambavyo **Mhe. Rais** amekuwa akisisitiza Taasisi za umma zibadilishane taarifa kidijitali.

**Ndugu washiriki**,

Mwaka uliopita wa 2023, mlikutana hapa katika kikao kazi cha tatu cha Serikali Mtandao na kuweka maazimio 12, ambayo Wizara iliyasimamia kwa ukaribu zaidi na kuhakikisha maazimio yote yanatekelezwa. Kama alivyotangulia kusema **Mkurugenzi Mkuu wa e-GA. Mha. Benedict Ndomba,** kupitia kikao hiki mtapewa taarifa ya utekelezaji wake.

Hivyo basi, tumieni muda huu wa siku tatu mtakazokuwa hapa katika Kikao kazi hiki cha nne cha Serikali Mtandao, kujadiliana na kuweka mikakati madhubuti ya kukuza na kuimarisha jitihada za Serikali Mtandao, kuanzia ngazi ya chini yaani Serikali za Mitaa hadi ngazi ya juu ya Serikali Kuu. Kwa muktadha huo, natumaini kuwa mtatoa mawazo na michango yenye tija itakayowezesha Serikali kutekeleza na kuimarisha jitihada za Serikali Mtandao.

Niwahakikishie kuwa, Wizara itasimamia utekelezaji wa yale ambayo mtakubaliana nayo ili kuhakikisha huduma za Serikali Mtandao zinafika kila sehemu, kuanzia mijini hadi pembezoni mwa miji.

**Ndugu Washiriki**, nikiwa ndiye Waziri mwenye dhamana ya kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan,** kutimiza dhamira yake ya kuujenga utumishi wa umma wenye uadilifu na unaowajibika kwa wananchi, mimi na msadizi wangu **Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb),** pamoja na watendaji wanaotusaidia kutekeleza wajibu wetu, tutahakikisha tunaisimamia na kuiongoza e-GA katika kuimarisha Serikali Mtandao, kwa kubuni na kusanifu mifumo ya TEHAMA ambayo itawezesha kutimiza azma ya **Mhe. Rais** ya kuujenga utumishi wa umma wenye uadilifu na unaowajibika kwa wananchi kwa kutoa huduma bora.

**Ndugu washiriki**, mwisho lakini si kwa umuhimu,nitumie fursa hii kutoa wito kwa viongozi, watumishi wa umma na washiriki wa kikao kazi hiki pamoja na wananchi kwa ujumla, kuunga mkono kwa vitendo kaulimbiu ya **KAZI IEENDELE** ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** ili kwa pamoja tulijenge taifa letu.

**Ndugu Washiriki,** Mabibi na Mabwana, nihitimishe kwa kurudia tena kuwashukuru na kuipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kuandaa Kikao Kazi hiki muhimu.

Nawashukuru pia wageni waalikwa kwa kuhudhuria Tukio hili muhimu. Ni matumaini yangu kuwa, mtatumia kikao hiki kutoa

mawazo muhimu, ambayo yatasaidia kukuza na kuimarisha jitihada za Serikali Mtandao. Hivyo, niwasihi mshiriki kikamilifu kwa kutoa mawazo chanya yatakayosaidia kujenga mifumo na miundombinu imara ya Serikali Mtandao.

Baada ya kusema hayo, sasa natamka kuwa Kikao Kazi cha Nne cha Serikali Mtandao kimefunguliwa rasmi.

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**